# *SEMA NA MWAMBA HUU*

Bwana awabariki. Mnaweza kuketi. Ninasikitika kwamba hatuna majuma mengine kadhaa ya huu. Ninataka kusema ya kwamba huu umekuwa mmoja wa miamsho ama mikutano mizuri sana, niliyopata kuwa nayo. U—unaonekana kuwa ni sikukuu kwangu mimi, mkutano huu. Sijawahi kuwa na wakati maishani mwangu ambapo nimewahi kuwa na uhuru zaidi, na nikajisikia huru zaidi kuhubiri tu imani yenyewe ya moyo wangu, kuliko kile nilicho nacho katika mkutano huu. Na umekuwa wakati mzuri sana.

2 Tulikuwa na wakati mzuri sana kwenye ushirika wa Wafanyabiashara, na pia wakati mzuri sana huko chini kwenye kanisa la Ndugu Sullivan asubuhi ya leo, nasi tumekutana na watu wengi sana wazuri, na hakika tunathamini haya yote.

3 Nasi tunataka kuwaambia, kama ikitokea kuna baadhi ya wa—watu waliopo, na kama hawapo, ninyi mnaoshughulikia hayo, tunataka kuwashukuru watu walioturuhusu kuchukua uwanja huu, hii Chautauqua. Tunathamini hilo, rafiki zangu. Na udumu kwa muda mrefu kwa kusudi la kumtumikia Bwana. Sasa, tunauthamini kwa mioyo yetu yote.

4 Ninataka kumshukuru Ndugu Sullivan, wachungaji wote wanaoshirikiana, ninyi nyote watu wapendwa, kwa yote mliyonifanyia. Kwa ajili ya matoleo ya upendo, na yote ambayo ninyi...Walisema walichukua moja muda mfupi uliopita, Ndugu duPlessis ndiyo kwanza aniambie. Nami ninawasalimu ninyi nyote na kuwashukuru kwa niaba yangu mwenyewe, mke wangu, mwanangu, Ndugu David duPlessis, Ndugu Sullivan, Gene, Leo, wafanyakazi wote, bila shaka tunawashukuru sana.

5 Tunawaalika kwa moyo mkunjufu, ya kwamba kama wakati wowote mkiwa na shida zozote, ama chochote ambacho tungeweza kuwasaidia, mbona, usiku hauingii giza kupita kiasi, wala mvua hainyeshi kupita kiasi, mngeweza kutuita... Nilikuwa nikisema ningeweza kuja kwenu, bali kuna wengi sana sasa, nisingeweza kufanya hivyo, maana imefikia, vema, nadhani mamilioni, sio kama tu hapa, bali kote ulimwenguni, mnaona. Nalo linalifanya gumu sana, si—siwezi kusema hivyo, ningependa kufanya hivyo, bali siwezi kulisema kwa moyo wangu wote, kwa sababu nisingeweza kulitekeleza.

6 Lakini kama una haja ya maombi, nitumie tu wakati wowote, tuma tu kwa: William Branham, Jeffersonville, Indiana. Huninii...Ofisi ya Posta 325, bali si lazima uwe nayo, itakuja, kwa vyovyote vile. Nasi tutafurahia kuwahudumia, kuwatumia vitambaa vya maombi, msaada wowote, chochote tuwezacho, bure kabisa, hakuna kitu, hakuna malipo kwa chochote.

7 Tuna vitabu, wanaviuza, na ni vya mtu mwingine. Ndugu Lindsay anamiliki kimoja cha hivyo, na Ndugu Julius Stadsklev anamiliki kingine. Nasi tunavinunua kwa kupunguziwa senti arobaini kwa kitabu, ndipo inatubidi kulipia kuvileta, tulipie kuviuza, tukastahimili hasara, nanyi mnaona jinsi tulivyo? Sikuzote tunapata hasara kwa hivi vitabu. Kila wakati tunapovifanyia hesabu, daima tumepungukiwa.

8 Kwa sababu nimewaambia hawa wavulana, na wote, wakimwona mtu yeyote anayetaka kitabu, wala hawana pesa za kukilipia, wakichukue, kwa vyovyote vile, wachukue hicho kitabu, kwa vyovyote vile. Nami niliona usiku wa kwanza tulipoanza mambo ya vitabu, maskini mama mkongwe amesimama kule nyuma, akipekua-pekua mfukoni mwake, akijaribu kupata senti sitini, hakuwa ila na arobaini.

9 Nikamwangalia yule mama aliyekuwa akiuza vitabu, kasema, "Vema, vinauzwa senti sitini." Nikakaribia moja kwa moja, nikamchukulia viwili ama vitatu, nikampa. Mnaona? Kwa hiyo, nami ninajua . . . Vipi kama huyo alikuwa ni mama yangu? Na jambo lingine, hivi vitabu si vya biashara, ni vya kujaribu kumsaidia mtu.

10 Hao wavulana wanauza kanda kule chini. Na hapa wakati mmoja, niliwachunguza hao wavulana, Gene na Leo. Gene ni mvulana wangu wa kanda, Leo ni katibu wangu wa huku nje. Nao wana santuri na kanda, basi niliwachunguza hao wavulana mimi mwenyewe nione wanauza hizo kanda kwa bei gani, maana nilinunua kanda kutoka kwa mwi—mwinjilisti mmoja iliyonigharimu karibu dola sita. Hao wanapata dola mbili na kitu kwake. Kwa hiyo niliona kile walichozilipia, nao ni, wanapata faida ndogo tu. Nao wanapata, niliwaambia wachukue kanda iliyo bora kabisa wanayoweza kupata, nao wanatumia kanda ya Scotch. Wanazo kanda hizo, Ujumbe wowote, ama chochote . . .

11 Na sasa, wakati mwingine . . . Ninataka kuliweka jambo hili dhahiri. Sasa kila mtu ana wazo lake mwenyewe, tuna fundisho lako mwenyewe, wakati nikiwa huku nje katika mchanganyiko wa madhehebu, ninajaribu kulishikilia kwenye yale Mafundisho makuu ya kimsingi, ya kiinjilisti, kwa sababu ya ndugu wengine wahudumu, nami ninataka ndugu wahudumu wajue jambo hili. Wakati mwingine katika kanisa langu mwenyewe, ninahubiri imani yangu mwenyewe kuhusu mambo, sasa, mle ndani kuna watu wengi wanaochukua kanda, na wakati mwingine zinatoka nje.

12 Sasa, nisingetaka kumsukumia mtu yeyote chochote nilichoamini, kitu fulani kidogo tu nilichokuwa nacho niani mwangu mwenyewe, na nikawazia kilikuwa *hivi*. Na kama sikulifundisha jinsi nilivyoliwazia, ningekuwa mnafiki. Kwa hiyo ninaiacha tu sehemu hiyo, ninaenda na kuhubiri yale

ninayojua kwamba hao wengine wanakubaliana nayo, mnaona, na kuendelea.

13 Lakini sasa, kama ikitokea upate, baadhi ya washiriki wako, ndugu, upate kanda inayotoka kanisani kwangu, juu ya jambo fulani ambalo huenda usikubaliane nami, tafadhali usinichukie juu yake, mimi ni ndugu yako, na—nawapenda. Na si—sikusudii zitoke nje, lakini huwezi kulizuia wakati kuna ishirini ama thelathini wanaochukua kanda, na kadhalika, mnaona. Na kwa hiyo, tunajaribu kulizuia vizuri tuwezavyo. Kanisa lilijichukulia jukumu, ule wakfu, ku—kujaribu kuwaweka hao wavulana peke yao wakati wanaporekodi kanda kwenye mikutano yangu.

14 Na kwa hiyo, niko hapa kushirikiana, kuufanya Mwili mmoja mkubwa wa Yesu Kristo, hivyo tu. Na hata hivyo, sehemu yake kuu ya msingi ni toba, na ubatizo, na imani kwa Mungu, wokovu, uponyaji wa Kiungu, nami nafikiri sisi sote tunaweza kukubaliana juu ya jambo hilo, mnaona, juu ya mambo hayo.

15 Sasa, kuliendea jambo hilo wakati mwingine, huenda nikawa na mtazamo tofauti kidogo, lakini nafikiri hivi... Wakati mmoja nilikuwa kazini mwangu Jeffersonville, nilikuwa nikifanya kazi katika Kampuni ya Utumishi wa Umma, na kulikuwako na—na Bw. Bohannan, huyo msimamizi alikuwa ni Mason Mkuu wa kitambo, nilikuwa mhubiri wa Kibaptisti, Kasisi Arnie Clegg kutoka Kanisa la Kimethodisti la Mtaa wa Maple akaja, halafu basi akaja Padre Halpin, yule kasisi wa Katoliki. Vema, naweza kunukuu aliyosema? Vema, alisema, "Tunapaswa kuanzisha mchezo wa kawaida, sote tuko hapa." Kasisi wa Katoliki alisema hivyo.

16 Na kwa hiyo, basi akafanya jambo fulani, hata hivyo, ambalo—ambalo lilianza kufingirisha jambo fulani moyoni mwangu. Akasema pale, akachora mistari mitatu, akasema, "Hii *hapa* Pennsylvania ikishuka, Billy," huyo alikuwa ni mimi, kasema, "utashukia njia hiyo. Na hii *hapa* nyingine, ya Kusini," kasema, "Bw. Clegg hapa atashukia njia hiyo. Hii *hapa* nyingine hapa." Kasema, "Dumu tu kwenye njia yako, kama zinaninii, mradi zinaelekeza Mbinguni." Nilifikiri hilo lilikuwa zuri sana kwa kasisi.

17 Basi akasema, "Dumu kwenye njia yako." Na hiyo ni kweli, mradi umeongoka na unamwamini Bwana Yesu Kristo, endelea tu kusonga mbele kwa moyo wako wote, Naye atakuongoza katika Nuru. Ninaamini hilo kwa yote yaliyo ndani yangu.

18 Wote ambao wamekuwa wazuri sana, kina mama walio na muziki, huo uimbaji maalum, kila kitu kimekuwa kizuri sana. Basi nadhani hawawezi kunisikia, lakini polisi ambao wamekuwa wakitusaidia huko nje, tukiingia na kutoka, tukiegesha magari, bila shaka wamefanya kazi nzuri sana, kazi nzuri. Kila mtu amekuwa mzuri sana, na hakika tunalithamini.

19 Na ni matumaini yetu, na maombi yetu, na shauku zetu, kwamba tumefanya jambo fulani, ama kusema jambo fulani, ama mumemwona Mungu akifanya jambo fulani kwa sisi, ambalo litaimarisha imani yenu, na litawafanya kumpenda Yesu zaidi, nawe ukiwa mgonjwa, kwamba utaponywa, maana hiyo ndiyo shauku ye—yetu rahisi, ya moyo mweupe, kwa kuwa hiyo ndiyo iliyotuleta hapa. Na kama tumefanikisha hilo kwa kuja kwetu, tunamshukuru Mungu kwa yote yaliyo mioyoni mwetu.

20 Na sasa, kama ukiwahi kuwa huko chini karibu na Jeffersonville, mbona maskini ile maskani ndogo iko kwenye Barabara ya Nane na ya Penn, mara moja moja niko mle, nikifanya ibada kule. Ama popote pale mikutanoni, hebu tukutane pamoja tena na kupeana mikono. Nami natumaini kuwa hapa tena mwaka ujao, Bwana akipenda. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni, asanteni.

21 Sasa, ni wangapi wenu watakaoniombea wakati niko nje hudumani? Hilo—hilo ndilo jambo muhimu. Mungu awabariki, hilo ni sawa. Mnaniahidi maombi yenu, na hiyo ni kusema, hizo ndizo nguvu zangu, ambapo ninazitoa kwa Mungu, ni kwa Roho Mtakatifu.

22 Kuna mambo mengi sana ambayo ningeweza kusema. Wengi wa marafiki zangu kutoka Jeffersonville wako hapa, na kutoka sehemu mbalimbali. Akina Downing wako hapa, kutoka huko chini Tennessee, sijawahi kuwaona, bali niliwapungia mkono. Ndugu Welch Evans, mke wake na familia wako hapa, mahali fulani, nisingeweza kuwaona sasa. Ndugu Banks Wood, baba yake, na mama, na ndugu, na wote ni Mashahidi wa Yehova walioongoka, nao wako humu m—mkutanoni. Na loo, nasikia ya kwamba Ndugu Hickerson alimpokea Roho Mtakatifu jana usiku, loo, Mungu asifiwe, yeye na mke wake. Ndugu Collins, mhubiri wa Kimethodisti, nanii wake. . .yeye, mke wake, na ndugu yake na—na mkewe, wote walimpokea Roho Mtakatifu. Na loo, nawaambia, mambo yanafingirika tu, kiajabu.

23 Kisha tunawashukuru ninyi watu wapendwa mliokuwa kwenye vyumba vya maombi kusaidia kuomba pamoja na watu hawa; inamaanisha mengi kwa kanisa langu kuimarishwa hivyo. Mtu fulani aliniambia ya kwamba Ndugu Wood na hao wengine walikuwa wamempokea Roho Mtakatifu pia, ambao walikuwa wakiutafuta huo ubatizo. Ninashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Bwana na awabariki ndugu hao. Nami najua kutakuwa na kitu kipya maishani mwao, kitakuwa halisi. Amina.

24 Sasa, tutawaombea wagonjwa. Hatutaki kuwaweka muda mrefu sana, tunawatakeni mrudi kanisani mwenu, usiku wa leo. Kama unazuru, mbona, tembelea baadhi ya haya makanisa.

25 Ndugu David duPlessis ndio kwanza atoe taarifa, na kusema walikuwa na wakati mzuri sana mahali walipokuwa asubuhi ya

leo. Nami nilikimbilia kwa Ndugu Sullivan nasi tulikuwa na wakati mzuri sana kule pamoja na kusanyiko lake.

26 Maskini ndugu huyu hapa, sijaninii...Ndugu Pat Tyler ni mwingine wa ndugu zangu na wenzangu. Naam. Ndugu Anthony kutoka New York, maskini...Je, wewe ni Myunani, ndugu, ama...? Mwitaliano. Kanisa dogo la Kiitaliano huko New York. Kila mahali, wengi sana kila mahali, kamwe nisingeweza kuyataja majina yao, bali na—natumaini ya kwamba Mungu atawabariki sana.

27 Sasa, kila mtu aliye hapa ambaye hajaponywa, hebu hii iwe ndiyo saa, hebu huu uwe ndio wakati. Sasa, jana usiku kulikuwa na lundo la viti vya magurudumu hapa, nami ni—nilikuwa chini ya upambanuzi sana, mpaka ni—ni—nisingeweza kuliona kusanyiko tena, na karibu nianguke kwenye vipandio huko nje nikitoka. Nami niliendelea kumhisi Billy, ama mtu fulani akinigusa pande zote niondoke.

28 Lakini mimi, kulikuwa na maskini mtoto mchanga mwe—mweusi, ambaye nilivutiwa naye sana. [Ndugu mmoja anasema, "Yuko papa hapa."—Mh.] Yuko hapa. Nilikuwa nimeona kile kilichokuwa kimempata huyo mtoto, kosa la daktari ambaye alileta ma—madhara akimdunga sindano. Lakini na—naamini ya kwamba mtoto huyo atakuwa mzima. Hiyo ni kweli.

29 Nami ni—nilikuwa nimedhoofika sana, hata nisingeweza kuita tena. Kama...Watu kamwe hawatajua mpaka nitakapokutana nanyi katika Nchi ile, kile hilo hunifanyia mimi. Mnaona? Wewe...Ni vigumu tu, ndugu, dada. Hamwe-...

30 Wazieni tu, Yesu wa Nazareti, mwanamke mmoja aligusa vazi Lake, Yeye alisema hilo lilimfanya dhaifu, nguvu zilimtoka. Hiyo ni kweli? Na huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Na kusimama hapa na kuliona wakati, baada ya wakati, baada ya wakati. Njia pekee ni kwamba, ni kwa sababu Yeye aliahidi, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya; nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu." Ninajua inasema *kubwa zaidi*, lakini tafsiri sahihi kutoka kwake ni *nyingi zaidi*. "Nyingi kuliko hizi mtazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu."

31 Sasa, kabla hatujasoma Neno la Baba, hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi.

32 Baba yetu Mwenye Neema na Upendo, Mheshimiwa, tunakuja Kwako tukiwa wanyenyekevu kadiri watoto wangeweza kuja. Nasi tulikuwa tukiwapa ndugu zetu na marafiki zetu shukrani kwa yote ambayo wametufanyia katika mkutano huu. Sasa kila mmoja wetu pamoja, huku vichwa vyetu na mioyo yetu imeinamishwa, tunakushukuru Wewe, Baba yetu mpendwa, kwa wema Wako, kwa kuwa ilikuwa ni kupitia Kwako ambapo haya yote yametimizwa: wanaoteseka

wameponywa, wagonjwa wameponywa, wenye dhambi wamekuja Kwako wapate kuokolewa, na wale waliookoka wamekuja na wamejazwa na Roho Wako. Hujaacha jambo moja bila kulifanya ambalo tumelihubiri. Umethibitisha kila Neno kwa ishara zilizofuata. Nasi tunakushukuru kwa ajili yake, Baba.

33 Nasi tunajua ya kwamba ni mapenzi Yako kumponya kila mtu, na kumwokoa kila mtu, na kumjaza kila mtu kwa Roho Mtakatifu. Nasi tunaomba, Baba, kama kuna yeyote hapa ambaye ameachwa nje, jalia watambue saa hii, kwamba si mapenzi Yako kwamba waachwe nje ya chochote wanachohitaji, kwa sababu Wewe upo hapa, na uko tayari, na unataka, na unatamani kuwapa shauku ya moyo wao. Kwa kuwa wao ni watoto Wako, ambao uliwatolea Maisha Yako, Nawe uko radhi na tayari kuwasaidia.

34 Yabariki Maneno tunayosoma, na tunapozungumza, jalia Roho Mtakatifu aliyebarikiwa ayapeleke Maneno hayo kote kwenye kusanyiko hili na kuyazamisha katika kila moyo, sawasawa na haja zao.

35 Na tutakapomaliza ibada alasiri ya leo, ama tuseme, *Wewe* utakapomalizana na ibada alasiri ya leo, nasi turudi manyumbani mwetu, sehemu mbalimbali, na miji mbalimbali, na majiji, na majimbo, na hata mataifa mbalimbali, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau ile asubuhi ya kwanza ya Pasaka, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?" Nasi daima tutakupa sifa, Baba. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu. Amina.

36 [Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu Branham anasoma Hesabu 20:5-8—Mh.] . . .*wala hapana maji ya kunywa.*

> *Musa na Haruni wakatoka pale palipokuwa mkutano, wakaenda hata mlangoni pa hema ya kukutania, wakaanguka kifudifudi: utukufu wa BWANA ukawatokea.*
>
> *BWANA akasema na Musa, akinena,*
>
> *Twaa ile fimbo,. . .wakusanye mkutano, wewe, na Haruni ndugu yako, ukauambie mwamba mbele ya macho yao;* ***nao*** *utatoa maji* ***yake****, nawe utawatokezea. . .maji katika mwamba: na hivyo utawanywesha maji mkutano na wanyama wao.*

Bwana na ayabariki Maneno ya Biblia Yake.

37 Hapana shaka ilikuwa ni a—asubuhi yenye joto sana. Hawakupata usingizi usiku kucha, walikuwa wamekusanyika kwenye oasisi ndogo. Usiku kucha wanyama walilia, na fa—farasi wakalia, na watoto wakalia, nao watu wakanung'unika, hawana maji ya kunywa, nao walikuwa huko nje jangwani peke yao. Nao walikuwa wametafuta kupitia kwenye chemchemi

zote karibu na mahali hapo, nazo chemchemi zote zilikuwa zimekauka, wala hapakuwapo na maji.

38 Dhambi yao ilikuwa imewaleta katika hali hii. Walikuwa wamesahau yote ambayo Mungu alikuwa amewafanyia, na kuwatendea, nao walikuwa wameanza kumnung'unikia Mungu na nabii Wake. Nayo ilikuwa imewaleta huko nje kwenye nyika hii, ambayo ilikuwa ni jangwa, hakuna maji, hakuna chochote kwa ajili ya watoto wao, hakuna chakula, hakuna maji ya kunywa.

39 Ni jambo la kuchukiza sana wakati watu wanapotenda dhambi, mfano wa kushangaza sana wa siku hizi ulimwenguni. Kisha tunaona, pia, ya kwamba walikuwa wamesahau kwa urahisi ya kwamba Mungu aliyekuwa amewaahidi kuwapeleka kwenye ile nchi, alikuwa ni yule Mungu aliyetoa ishara hizo zote na maajabu na miujiza.

40 Kama tungeweza kusimama, laiti tungeweza, bali hatuwezi, kutulia kwenye hilo kwa dakika chache, Mungu hutoa ahadi, kisha anathibitisha ya kwamba atatimiza ahadi hiyo kwa kutimiza Maneno Yake yote na kujionyesha Mwenyewe kuwa yupo. Jinsi inavyopendeza kwamba Mungu anafanya jambo lile lile papa hapa kwenye hii Chautauqua! Lakini mnaona, ninii yetu. . .

41 Tuko njiani tukielekea Nchi ya ahadi. Mungu aliahidi kukidhi mahitaji yao yote kutoka Misri hadi nchi ya ahadi; Mungu aliahidi kukidhi mahitaji yetu yote mpaka tutakapoifikia Nchi ya ahadi. Wala kusingekuwako na ugonjwa wowote miongoni mwetu kama tungalitimiza ahadi za Mungu, bali tumetenda dhambi.

42 *Dhambi* ni nini? Hawakuamini. Kutokuamini ndiyo dhambi pekee iliyopo. Kunywa pombe, kuvuta sigara, kucheza kamari, kufanya uzinzi, hizo si dhambi, hizo ni sifa za—za kutokuamini. Mnaona? Haki ni sifa za wokovu.

43 Lakini watu wanaweza kuacha kuvuta sigara, kunywa pombe, na kadhalika, na bado wasiokolewe. Mnaona? Kwa hiyo dhambi ni alama ya kwamba mtu anayeitenda si mwaminio. Biblia ilisema, "Asiyeamini amekwisha kuhukumiwa tayari." Kwa hiyo kabla hujaninii. . .Kama kamwe hukusema uongo, hukuiba, wala kufanya lolote maishani mwako, bado wewe ni mwenye dhambi kwa kuanzia. Wewe ni. . .Huna nafasi nje ya Kristo, Yeye ndiye Njia.

44 Nao watu hawa walikuwa wamemwacha Mungu kabisa, Naye alikuwa amewakatia njia ya kupata maji na chakula chao. Na hilo linafanana sana na siku hizi, kwamba Mungu amekatilia mbali baraka kuu kutoka kwa kanisa ambazo Yeye aliliahidi kanisa, kwamba angekuwa pamoja nao, sikilizeni, angekuwa pamoja nasi, hata ndani yetu, hata mwisho wa njia, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Kamwe sitawaacha

wala sitawapungukia. Nitakuwa pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari," kotekote.

45 Sasa, "Kwa nini Yeye hayuko kanisani siku hizi?" watu waliwazia. "Yuko wapi Mungu yule wa historia, Mungu yule aliyefufuka?"

46 Yeye anawangojea tu watu Wake wamrudie na kujiweka sawa. Ndipo mtamwona Mungu wa historia akiingia, wakati watu watakapokuwa sawa.

47 Jinsi walivyokuwa wamesahau kwa urahisi, ya kwamba wakati yale mapigo yalipokuwa huko Misri kwamba walilindwa. Wakati kulikuwako na nzi kote juu ya kila kitu, hapakuwapo na nzi karibu nao; wakati chawa walipojaza vitanda vyote, nguo zote, na kadhalika, hakukuwa na hata chembe moja ya hizo juu yao; vyura walikuwa kwenye kabati na kila kitu kingine, kote katika hao wengine wasioamini, bali walikuwa wamelindwa, Mungu akionyesha rehema Yake.

48 Angalieni, basi wakati ule usiku wa mwisho na mkuu ulipokuja, Mungu alisema, "Hili ndilo pigo Langu la mwisho kwa Misri. Lakini kabla sijapiga pigo hili, sina budi kuwaleta watoto Wangu kwenye ulinzi." Basi kulikuwa na mwana-kondoo wa sadaka aliyechinjwa, nayo damu ikawekwa kwenye nguzo na vizingiti vya mlango, nalo kusanyiko likaingia chini ya damu.

49 Kumbukeni, hilo lilikuwa ndilo pigo la mwisho lililoipiga Misri. Na pigo la mwisho linalolipiga kanisa siku hizi ni lile lile lililokuwako, mauti ya kiroho. Kwa sababu kama vile Mungu alivyowaongoza kihalisi, Yeye hutuongoza kiroho. Nalo pigo la mwisho kwa a—adui ni mauti yanayopiga, na wote wasio chini ya Damu wametengwa na ushirika na Roho Mtakatifu.

50 Sasa, kwa hiyo tuna mauti ya kiroho makanisani, hiyo ndiyo ishara ya mwisho kabla ya ile saa ya ukombozi, ni ma—mauti ya kiroho. Hivi Yesu hakusema jambo lile lile? "Watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wasiowapenda walio wema, wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake, hao nao mjiepushe nao." Saa tunayoishi sasa, wakati ulimwengu wa kanisa umepatwa na mapigo na unakufa kifo cha kiroho.

51 Lakini Mungu aliwalinda, nao walikuwa wamesahau jambo hilo. Jinsi waaminio wetu wa Kipentekoste wanavyosahau jambo hilo haraka, pia, kwamba mliokolewa kwa neema Yake na kujazwa na Roho Wake! Katika wakati huu mzuri, wa ajabu sana wa kufa kwa kanisa, msisahau jambo hilo, kwamba Mungu aliyewapa Roho Mtakatifu kuishi kwake na kufanya safari hii yuko pamoja nanyi kila hatua ya njia. Tunalisahau upesi sana, ni vibaya sana.

52 Sasa, jinsi ambavyo Mungu aliwatoa, jinsi ambavyo katika usiku huo mkuu alipita juu yao, ile Pasaka kuu, na jinsi

alivyokuwa amewafanyia mambo haya makuu. Sasa, halafu basi jinsi walivyokuwa wameanza kulalamika baada ya kutoka nje. Walikuwa wamefika kwenye—kwenye Bahari ya Chumvi, Mungu alifungua njia wakati hapakuwapo na njia nyingine. Mungu akawa Njia yao.

53 Hivyo ndivyo nilivyoona maishani mwangu, ninapofikia mahali ambapo hapana njia, ndipo Yesu hufanya njia ambapo hapana njia ya kufanywa. "Mimi ndimi Njia, nitaninii...na Kweli na Nuru."

54 Sasa, tunaona ya kwamba Mungu alifanya njia wakati hapakuwapo na njia na akawakomboa. Sasa, natumaini mmevaa makoti yenu ya kiroho, sikilizeni, na wasiotahiriwa, ikimaanisha wasio na Roho Mtakatifu, wasiotahiriwa...Ni wangapi wanaojua ya kwamba Roho Mtakatifu ni tohara? Kama uliwahi kusoma Biblia yako, unajua hilo. Toha-...

55 Stefano alisema, katika ujumbe wangu asubuhi ya leo, aliwaambia hao makuhani na hao wengine, "Enyi msiotahiriwa mioyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu kama baba zenu walivyofanya." Roho Mtakatifu huutahiri moyo.

56 Na sasa, safarini, Mungu aliahidi kuwashughulikia, Naye kweli aliwashughulikia. Wala Yeye hashindwi kamwe. Ndipo basi, wakati wasioamini walipojaribu kuwaiga, walizamishwa.

57 Nanyi mlijionea wenyewe, watu wakiingia na kujaribu kuiga ama kutenda kana kwamba wana Roho Mtakatifu, tunaona kuwa si muda mrefu kabla hawajaingia kwenye lundo la takataka. Hiyo ni kweli kabisa. Huwezi kuiigiza, haina budi kuwa ni kitu halisi ulicho nacho wewe mwenyewe. Huwezi kuingia na kutenda kana kwamba wewe ni Mkristo, huna budi kuwa mmoja. Na njia pekee unayoweza kuwa mmoja ni kwa kuzaliwa.

58 Tumewasikia watu wakiingia na kunena kwa lugha, muda si muda mwajua, tunawaona hapa kwenye lundo la takataka. Hawakumpokea Roho Mtakatifu, walipata mchafuko wa lugha. Wao kamwe...Roho Mtakatifu humfanya mtu kile alicho kutoka moyoni mwake. Ana upendo wa kiungu.

59 Sasa, walikuwa wamesahau haya yote. Na hii...Waliacha manung'uniko yao makuu kwa Musa na kwa Mungu, wakiwakemea, "Kwa nini mkatuleta huku? Kwa nini inatubidi kukaa hapa? Afadhali nirudi Misri wakati wowote. Kwa nini hatukufia kule chini? Acheni Farao atuue, ni bora kuliko kuwa huko nje."

60 Kama hayo si kama malalamiko ya kanisa siku hizi! Kwa urahisi sana wanausahau mkono wa Mungu; kwa urahisi sana waliusahau. Sikilizeni, ni kitu gani kilichotukia? Loo, ni ajabu sana. "Afadhali tukafie huko chini."

61 Angalieni, watu hao walikuwa wameacha kula vitunguu na vitunguu saumu vya Misri, naye Mungu alikuwa amenyesha mkate kutoka Mbinguni, chakula cha Malaika, na kuwalisha nacho, nao walikuwa wangali wakilalamika; Mungu amewapa Kanisa Chakula cha Malaika, Roho Mtakatifu, na wangali wanalalamikia jambo fulani wakati wote, kila mara.

62 Waliacha vitunguu na vitunguu saumu wapate kula chakula cha Malaika, ambacho Malaika walitayarisha Mbinguni na kukimiminia chini, chakula walichokuwa wamekula, na bado walikuwa wakilalamika. Walikuwa wameacha mito ya kale ya Nile iliyojaa matope, wakinywa maskini maji hayo yenye matope, nao walikuwa wakinywa kutoka kwenye Mwamba wa kiroho wa wokovu safi na maji, nao walikuwa wakiyalalamikia. Naam, daima wakilalamika, kwa sababu nyakati ngumu kidogo ziliwapata.

63 Loo, hiyo ni mara tu unapopata jaribio lako la kwanza, ukaja mkutanoni, ukamwona Roho Mtakatifu, ukarudi nje na kuumwa na tumbo, ukasema, "Vema, labda kamwe sikuponywa." Aibu kwako! Hakika, uliponywa kama unaamini. Hisia zako hazina uhusiano wowote nalo, imani yako ndiyo tunayoangalia. Hiyo ndiyo Mungu aionayo, ni imani yako, si hisia zako. Yesu kamwe hakusema, "Uliuhisi?" Alisema, "Uliamini?" Hilo ndilo wazo.

64 Lakini waliwaacha waganga wenye majivuno wa Misri, huko chini wakisema, "Loo, sisi ndio madaktari, siku za miujiza zimepita," wapate kuwa pamoja na Tabibu Mkuu. Na safari ya miaka arobaini, mamia na maelfu ya watoto wachanga wakizaliwa, magonjwa ya kila namna, nao wazee, hapakuwapo na hata mmoja mnyonge miongoni mwao, wakiwa na huyo Tabibu Mkuu mmoja. Haleluya! Na bado wanalalamika.

65 Walikuwa wameondoka mahali hapo huko chini, ambako ninii. . . ambako walisema, "Siku za miujiza zimepita." Hapo ndipo mlipoondoka, mliondoka mahali hapo panaposema, "Siku za miujiza zimepita." Waliondoka huko wapate kuwa pamoja na. . . huku nje ambako ishara na maajabu hufuatana na mwaminio, na hata hivyo walikuwa wakilalamika. Hiyo si ni kama tu watu wa siku hizi?

66 Lakini badala ya hayo yote, mbele ya hayo yote, wakati Mungu alipoona rehema kwa ajili ya watu, Musa akaanguka kifudifudi, yule nabii, na kusema, "Bwana Mungu, hakika, wametenda dhambi. Lakini sikia ninii yao. . . Wape nafasi nyingine."

67 Nini kilitukia? Mungu alimwambia, "Ondoka uende huko nje, ukaseme na Mwamba, nao utatoa maji Yake."

68 Sasa, kama hiyo haikuwa. . . Je, mtu wa kimwili si angelichukua hilo kama upumbavu? Mwenye nia ya kimwili angefanya nini? Mbona bila shaka, ule Mwamba ulikuwa ndipo mahali pakavu sana nyikani. Vema, kama kutakuwako na maji

yoyote, yangekuwa kwenye chemchemi, sio huko juu kwenye Mwamba ule. Mungu hufanya mambo kinyume wakati mwingine kutokana na yale mwanadamu anayowazia kwamba ni sawa. Hiyo ndiyo sababu mwanadamu hana haki ya kuwaongoza watu wa Mungu, inahitaji Roho Mtakatifu kufanya hivyo kwa Kanisa lililojazwa. Bila shaka.

69 Sasa, wanasema siku hizi, "Kama kuna uponyaji wowote wa Kiungu na miujiza, ungekuwa katika kanisa letu Katoliki; ungekuwa katika Baptisti yetu; ungekuwa katika Methodisti yetu."

70 "Lakini Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Yeye alifanya nini? Ninii, alienda mahali pasipotarajiwa kabisa, ule Mwamba.

71 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, wanasema, "Sasa, uponyaji huo unafanyika mahali pa namna gani? Hayo maono yanatukia wapi?"

"Ni kundi la Kipentekoste."

"*Ah!* Tokeni huko. Kama kuna kitu kama hicho anachotoa Mungu, angekileta kanisani mwetu."

72 Mnaona? Vema, hivyo ndivyo ilivyo. Nini kilitukia? Kwa nini hakukuwako na maji? Kwa sababu chemchemi zao za kujibunia zilikuwa zimekauka. Hiyo ndiyo shida ya makanisa siku hizi, madhehebu yetu ya kujibunia na theolojia zimekauka. Lakini Mungu angali ana ile amri ya kusema na Mwamba, Nao utatoa maji Yake. Bila shaka.

73 Naam, ni upumbavu sana kwenda kule juu, inaonekana ya kipumbavu sana. Kwa nini mtu aondoke mahali pakubwa ashuke aende miongoni mwa kundi la wale wanaowaita watakatifu wanaojifingirisha? Anafanya nini? Anatii tu Neno la Mungu. Hivyo ndivyo Musa alivyofanya. Alitii yale Mungu aliyosema afanye, alinena na Mwamba, haidhuru lilisikika la kijinga jinsi gani, ama chochote kile, alinena na Mwamba, nao Mwamba ulikuwa utoe maji ya uzima kwa ajili yao.

74 Loo, jambo pekee linalotupasa kufanya siku hizi ni kama tu ilivyokuwa wakati huo, ni kusema na Mwamba. Haijalishi kama chemchemi zote zimekauka, kama mengine yote yamepotea na kutoweka, jambo pekee tunalopaswa kufanya bado ni kuendelea, na kusema na Mwamba. Nao Mwamba ungali unaweza kutoa maji Yake. Mnaamini hilo?

75 Sasa, wakati mmoja katika Biblia. . . Sasa, tunapata mvua kidogo huko nje, pia, kwa hiyo ingieni tu ndani, mwiname kidogo hasa upande *huu* ambapo mvua inatokea, wala haitadhuru chochote.

76 "Sema na Mwamba, nao Mwamba utatoa maji *Yake*." Mliona jambo hilo? "*Huo*," h-u-o, "*huo* utatoa ninii *Yake*," kiwakilishi

nafsi, "maji *Yake*." Maji ya aina gani? Maji ya Uzima, utatoa ya aina hiyo. Mungu aliahidi, na Mungu atafanya hivyo.

77 Sasa, hiyo ndiyo shida siku hizi. Unapokuwa umeenda umbali uwezao kwenda, kama umetafuta katika kila ofisi ya daktari iliyopo, na wangali wanasema hakuna kitu unachoweza kufanyiwa, basi nitakwambia, fanya kama Musa alivyofanya, sema na Mwamba, kwa kuwa ungali unaleta maji Yake ya wokovu na uponyaji wa Kiungu, kama tu vile Mungu alivyoahidi. Jambo pekee likupasalo kufanya, kama daktari akisema la, sema na Mwamba Nao utatoa maji Yake.

78 Sasa, Hana . . . Hajiri alifukuzwa nyumbani kwake. Alikuwa na mtoto mchanga, maskini jamaa huyo alikuwa yuafa. Mbona, hakujua la kufanya naye. Hakuelewa jinsi bibi yake alivyo—alivyomtendea. Nini kilitukia? Walipopatwa na hali hii, maskini ulimi wa mtoto wake mchanga, ulimi wa maskini Ishmaeli, ulikuwa ukivimba ukimtoka. Akamlaza chini ya kichaka, akatoka kadiri ya mtupo wa mshale akaanguka kifudifudi, naye akasema na Mwamba, nao Mwamba ukatoa maji.

79 Basi kulikuwako na chemchemi, Beersheba, ambayo ingali inasimama leo kama kumbukumbu ya milele kwamba Yeye angali ni Mungu, nawe unaweza kuzungumza Naye, Naye ataleta chochote unachohitaji, kila kitu alichoahidi nchini. Hakika.

80 Wale wana wa Kiebrania walitaka kudumu waaminifu kwa Mungu. Siku moja kwa sababu walikuwa waaminifu kwa Mungu, serikali ya shirikisho iliwatoza faini, nao wakasema wangewatupa katika tanuru ya moto, ambayo ilimaanisha kifo cha papo hapo. Ndipo walipoanza kuwatupa katika tanuru ya moto, walikuwa wameomba usiku kucha, wakamtafuta Mungu, nao walipowatupa katika tanuru ya moto, waliwaacha waungue kwa yapata saa nne ama tano. Mfalme akashikwa na wasiwasi, akasema, "Nendeni, mkaufungue mlango."

81 Basi walipoufungua huo mlango, waliwakuta wale wana watatu wa Kiebrania wameketi mle ndani, wakisema na Mwamba, ulioweza kuwaokoa na ule moto katika hiyo tanuru. Walikuwa wakiunenea Mwamba, nao Mwamba ulikuwa umeuzima huo moto.

82 Yoshua, siku moja alihangaika, Mungu alikuwa amemwongoza kuvuka bahari, na . . .?. . . kuvuka mto Yordani. Alikuwa anaendaje kuiteka nchi hii? Alikuwa anaendaje kuiteka Yeriko? Alikuwa akitembea huku na huku alasiri moja, akijaribu kuwazia jinsi ambavyo angeweza kupanda hizo kuta, ama chochote kile. Baada ya kitambo kidogo, akamwona Mtu amesimama pale, akauchomoa upanga wake akaenda kumkabili, huyo Mtu akauchomoa upanga Wake akaja kukabiliana naye. Akasema, "Je, Wewe uko upande wetu? Je, uko upande wa adui zetu?"

Akasema, "Mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana."

83 Yoshua akaunenea huo Mwamba, nazo kuta zikaanguka. Mradi tutazungumza na Mwamba, kutakuwako na njia itakayotengenezwa.

84 Bartimayo kipofu, mamia ya miaka baadaye, alikuwa ameketi, sasa angalieni, mamia na mamia ya miaka baadaye, maskini mzee kipofu aliketi kando ya ukuta, akiota juu ya siku ambazo Yoshua alizitikisa hizo kuta kwa nguvu za Mungu, akiketi pale katika upofu wake, naye akasema, “Loo, laiti ningaliishi katika siku hiyo, ningalimwona Yeye, pia.”

85 Ndipo chini ya dakika chache tangu wakati huo, maskini Bartimayo kipofu, bila matumaini, bila tiba yoyote ya kimatibabu, bila chochote, akanena na Mwamba, nao Mwamba ukamrejeshea macho yake. Wakati Yesu wa Nazareti, ambaye ni Mwamba katika nchi yenye uchovu, Yeye alinena naye, Naye akayafumbua macho yake.

86 Yule mwanamke kisimani, alikuja kule siku moja kunywa maji. Maisha yake yalikuwa yakimhukumu, alitaka maji, ndipo akashusha chini kuyateka. Mtu fulani aliyeketi pale akasema, “Kwa nini usiniombe Mimi maji unywe? Ningekupa Maji usije hapa kuteka.”

87 Naye akasema, “Bwana, nipe Maji haya milele.” Aliunenea ule Mwamba, naye alipoyanywa maji hayo, alikimbia mjini, akisema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Hakika, alikuwa na kiu, naye akanena na Mwamba.

88 Martha, dada yake Lazaro, siku moja ugonjwa ulipokuwa umekuja nyumbani mwao, mauti yalikuwa yamekuja nyumbani mwao, ndugu yake alikuwa amekufa, amezikwa, akinuka huko kaburini, bali akashuka kwenda mjini, kwa kuwa alisikia kitu fulani, “Imani chanzo chake ni kusikia,” basi alipofika kule chini, akaunenea Mwamba. Ndipo ule Mwamba ukamfufua tena ndugu yake aliyekufa, kwa sababu aliunenea Mwamba, nao Mwamba ukarudisha uhai wa huyo mvulana aliyekufa.

89 Wanafunzi usiku mmoja katika dhoruba mbaya mara mbili kuliko hii, walikuwa huko nje kwenye bahari yenye dhoruba kali, na matumaini yote yalikuwa yamekwisha. Walifikiri wangeangamia, lakini ilitokea walikumbuka, walikuwa na huo Mwamba kwenye meli. Haleluya! Wakanena na Mwamba, nao Mwamba ukatoa maji Yake ya Uzima wa Milele. Basi akanena na pepo na mawimbi, nayo yakamtii. Iliwabidi tu kusema na Mwamba.

90 Kama unahitaji furaha, unenee Mwamba; kama unahitaji wokovu, sema na Mwamba; kama unahitaji uponyaji wa Kiungu, unenee Mwamba; kama unahitaji Roho Mtakatifu, unenee Mwamba, Naye ataleta maji Yake, maji ya wokovu, kama tu utaunenea Mwamba. Chochote unachohitaji, sema na Mwamba.

91 Mwamba ni yeye yule leo kama alivyowahi kuwa, angali ana Uzima wa Milele, angali ana amani ya Milele, angali ana furaha isiyosemeka na iliyojaa utukufu, angali ana uponyaji wa Kiungu. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Jambo pekee watu wanalohitaji kufanya ni kuunenea Mwamba. Amina! Mnaamini hilo?

92 Na tuinamishe vichwa vyetu basi, na tuunenee Mwamba, kila mtu katika maombi.

93 Baba wa Mbinguni, tunakuja katika Jina la Mwamba, Mwamba katika nchi yenye uchovu, Kimbilio wakati wa dhoruba. Tunaomba, Ee Bwana Mungu, ya kwamba Mwamba utatutia uvuli kwa nguvu Zake na rehema, hata Huo... kila mgonjwa hapa ndani aweze kuponywa leo, jalia waseme na Mwamba. Kuna wanaume na wanawake walioketi hapa wakiugua kansa, baadhi yao vipofu, na wengine viwete, daktari anasema hakuna tumaini kwao, basi hebu na waunenee Mwamba.

94 Musa bila tumaini, walikuwa nyikani ambako hakukuwa na maji, bali wakaunenea Mwamba, nao Mwamba ukatoa bubujiko, nao wote wakanywa, wakaishi. Bwana Mungu, jalia tunywe leo kutoka kwenye chemchemi hiyo isiyokauka, loo, katika Nchi hii ya Fahari Kuu ya wokovu, ambamo tumeitwa tutoke kwenye vitunguu saumu vya Misri na vyombo vya uvundo, tuingie mahali hapa pazuri sana ambapo ni Nchi ya Fahari Kuu sana, ulipo ule Mwamba, tukila Chakula cha Malaika na kuinywea Chemchemi isiyokauka kamwe.

95 Mungu uliye Mbinguni, wajalie watu hawa baraka hii. Jalia waone, leo, ya kwamba ule Mwamba ungali hai, ule Mwamba uliofufuka katika wafu, ule Mwamba umo humu nchini leo. "Yeye ni Kimbilio wakati wa dhoruba, na jalia watu wakimbilie Humo wawe salama." Tujalie, Bwana. Yasikie maombi ya watumishi Wako tunapoomba na kukuita Wewe. Katika Jina la Mwanao Yesu Kristo. Amina.

96 Loo, jamani, unenee Mwamba. Kama wewe ni mgonjwa, nena na Mwamba. Kama daktari akisema, "Siwezi kukufanyia la zaidi," basi nenea Mwamba. Kama kanisa likisema, "Ukipaza sauti kanisani mwangu, nitakufukuza," basi nena na Mwamba. Kama dhehebu linataka kukufukuza, unenee Mwamba. Amina. Mauti yanapokuja kuiba chumbani mwako, nena na Mwamba, Yeye atafanya njia na kuyagawanya maji ya Yordani kama alivyowafanyia, nanyi mtatembea juu ya nchi kavu.

97 Nena na Mwamba, hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya, haikubidi kuupiga tena, nena Nao tu, liitieni tu Jina Lake, "Lolote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, hilo nitalifanya." Amina. "Nena na Mwamba, Nao utatoa maji Yake."

98 Nena Nao, waangalie wengine wakinena Nao. Nyinyi msio na Roho Mtakatifu, waangalieni hao walionena Nao, Wamethodisti, Mashahidi wa Yehova, Wabaptisti, wote kama hao. Nena na Mwamba, Mwamba hauna upendeleo wa mtu, hauna upendeleo wa wakati, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na daima atakuwa Mwamba ule ule ulioahidiwa kutupatia yote tunayohitaji, kuanzia hapa hadi kwenye Nchi ya ahadi. Amina. Unaamini hilo?

99 Mligawa kadi za maombi? [Ndugu Billy Paul anasema, "C."—Mh.] Huh? ["C."] Billy alisema waligawa kadi za maombi. Vema, hebu tuone. Ninyi wagonjwa, njoni alasiri ya leo, njoni mkifanya hivi: mkiwa katika hali ya kunena na Mwamba. Mimi sio ule Mwamba, mimi ni mlango Wake tu. Mnaona?

100 Huduma zetu ni vituo tu ambapo, ni bomba ambamo maji yanapitia. Usitukuze hilo bomba, yatukuze maji unayopata kwenye hilo bomba, kwa maana hayo maji hutoka kwenye ile Chemchemi. Yatukuze hayo maji. Kisha kumbukeni, isingeweza kuwa ni mimi niliyeponya, bomba halikunyweshi, shina yanalopitia, halikunyweshi, hutoa tu maji. Unaunywea Mwamba huo, Mwamba huo uliopigwa, ambao tayari umepigwa.

101 Musa aliupiga Mwamba huo kwa fimbo ya hukumu ya Mungu, ndipo hukumu za Mungu zikaupiga huo Mwamba, Kristo Yesu. Halafu Musa alipoupiga huo Mwamba, kulikuwa na ufa katika huo Mwamba, daima kulikuwako na ufa katika Mwamba huo tangu wakati huo na kuendelea; na wakati Kristo alipopigwa, kulikuwako na ufa katika huo Mwamba.

102 Kutoka kwenye Mwamba huo, walipata asali walipokuwa na njaa, walipata maji walipokuwa na kiu, kwa kuwa ulikuwa ni Mwamba uliopigwa. Mwamba uo huo leo una maji na asali, na Uzima kwa wingi, furaha isiyoneneka iliyojaa utukufu, uponyaji wa Kiungu, nguvu za Mungu kumweka mtu huru na dhambi. "Sema na Mwamba, *nao* utatoa maji *Yake*." Amina.

103 Vema, wale walio na kadi za maombi (Ilikuwa nini? C, moja hadi hamsini.), pangeni mstari upande huu. Loo na—najisikia kusema na Mwamba, nanyi je? Nina furaha sana kwamba kuna Mwamba. [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Huh? C. Yule mama pale alisema . . . Hiyo ni kweli? [Dada mmoja anasema, "Kadi ya maombi C."—Mh.] C, naam, C. Vema.) C, moja hadi hamsini.

104 Loo, nena na Mwamba. Loo, nilimsikia jamaa mmoja akiimba wimbo hivi majuzi usiku, "Ninautafuta Mwamba ulio juu kuliko mimi." Huo ndio Mwamba tunaotaka kuuona.

105 Sasa kumbukeni, mnasema, "Laiti ningaliweza kusema na Mwamba!" Mwamba hunena Mwenyewe. Whiu! Laiti ningalikuwa mkubwa kuliko nilivyo. Mwamba hujitetea Wenyewe. Ni wangapi wanaamini hilo? Mwamba si bubu,

Mwamba huu ni Mwamba ulio hai. Ninyi ni mawe yaliyo hai, yaliyounganishwa pamoja na Mwamba huu kufanya kimbilio.

106 "Nena na Mwamba, nao Mwamba utatoa maji Yake. Ashukuriwe Mungu aliye hai atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Nampenda.

107 Sasa, wanapojitayarisha, ni wangapi hapa ambao hawana kadi ya maombi, nanyi mnataka kusema na Mwamba? Loo, jamani, hilo ni sawa. Sasa, Mwamba hauko tu katika mstari huu wa maombi, Mwamba unawafunika wote.

108 Hebu na tuimbe sasa, wimbo mzuri, *Nampenda*, tafadhali, dada, tupe sauti. Wakati tunapowangojea wapate kuwapanga watu wasije wakasongamana, kwa namna fulani wapangwe mstarini, hebu na tuimbe sasa kwa moyo wetu wote sasa.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Na . . .

Hebu tuinue mikono yetu.

. . . nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Loo, jinsi ninavyoupenda huo! Nanyi je? [Ndugu Branham anavumisha *Nampenda*—Mh.]

Mtini Kalvari.

109 Ni ajabu jinsi gani, tukufu! Sasa, hebu na tuombe dua kidogo Kwake. (Endelea tu, dada.)

110 Ee Mungu, Baba yetu wa Mbinguni, wakati upako wa Roho Mtakatifu Wako unapoingia juu yetu, basi tunaonekana kusahau ya kwamba tungali ni wa duniani. Inaonekana kuna hisia ya ndani zaidi ya—ya kitu kilicho halisi zaidi, inatufanya kulia na kupaza sauti, na mambo makuu, ya ajabu sana tunayofanya ambayo ni magumu kueleweka kwa nia ya kimwili, bali tumesema na Mwamba.

111 Ni ajabu sana kuwazia ya kwamba—ya kwamba Mwamba ungeleta maji, bali kulikuwako na maji pale mahali fulani, kuzifuata amri za Mungu daima huleta matokeo. Nasi tunakushukuru kwa ajili ya jambo hili, Baba yetu.

112 Nasi tunaomba sasa, ya kwamba tunapomalizia uamsho huu na ibada, kwamba hakutakuwa na mtu mmoja hapa, ila atakayepokea yote yaliyowaleta. Kama ni kwa ajili ya wokovu, jalia wakukubali Wewe kama Mwokozi wao binafsi. Kama bado hawajazaliwa mara ya pili, wakajazwa na Roho, tunaomba ya kwamba watajazwa na Roho Wako. Kama ni uponyaji, jalia

kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu mwishoni mwa ibada hii.

113 Wabariki, Bwana, wamekuja, wameketi huku, wamengojea, na Bwana, sijui ni lipi la zaidi tungeweza kufanya, kuhubiri, kuwaambia Kweli, kuyasoma kutoka kwenye Maandiko, kuwapa mifano, halafu zaidi ya hayo yote, Wewe unashuka moja kwa moja katikati yetu na kuthibitisha ya kwamba Wewe upo hapa. Jalia wawe na imani ya kusema Nawe alasiri ya leo, na kusema, "Bwana, niponye, niokoe, nijaze na Roho Wako." Tujalie, Bwana. Tunawakabidhi wote Mikononi Mwako sasa. Katika Jina la Bwana Yesu. Amina.

[Ndugu fulani anatoa tangazo—Mh.]

114 Sasa, tunapotulia na kujituliza, wakati huu mkuu mtakatifu tunaokabili sasa, hapa ndipo ambapo mahubiri yote ambayo nimehubiri na kadhalika, yataonekana kuwa ni sahihi au si sahihi. Sasa, kama huo mwamba uliishi tu nyikani, wala si mwamba ule ule leo, basi hauta—hautanena, bali kama ni Mwamba ule ule, Yeye atanena kwa Neno lile lile. Hiyo ni kweli? Hakika, ndivyo alivyo.

115 Alisema, "Baba zetu walikula nyikani, chakula."

116 Akasema, "Lakini Mimi ndimi Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni, mwanadamu hula Hiki wala hafi kamwe." Kisha akasema, "Kwa nini . . . " kuhusu Musa na—nao wakawaambia . . . Yeye aliwaambia Musa asijakuwako, Yeye alikuwako.

117 Naye ni Mwamba ule ule mkuu. Wakati alipokuwa hapa ulimwenguni katika Mwili wa nyama, akakaa ndani ya Mtu mmoja, Mwanawe Kristo, tunaona yale aliyofanya katika siku hizo, Yeye kamwe hakufanya chochote hadi alipoona maono afanye nini. Hakuna mtu . . . Yeye alisema Mwenyewe . . . Ni watu wangapi wanaojua ya kwamba Yesu alisema Yeye hakufanya lolote, mpaka alipoliona likitendwa kwanza? Kama ukitaka kulisoma, Yohana Mtakatifu 5:24, ama, 5:19, samahani, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile."

118 Sasa, hiyo ama ni kweli au si kweli. Kama ni kweli, Yeye kamwe hakufanya mwujiza mmoja, ama kufanya jambo moja, mpaka Mungu alipomwonyesha kwa ono, kwanza, la kufanya, hivyo ndivyo alivyosema, la sivyo Yeye alisema uongo, asingeweza kufanya hivyo na kubaki Mwana wa Mungu.

119 Sasa, najua itakuwa vigumu kidogo kwenu kusikia. Nami nitawaomba wahandisi, chochote walicho, waongeze tu hizo maikrofoni sauti sana wawezavyo. Kwa sababu chini ya ono, hujui unachosema, hata hujui mahali ulipo. Kwa hiyo basi, hili hapa.

120 Sasa, kuna mtu yeyote hapa ambaye hajawahi kuwa katika mmoja wa mikutano hapo kabla? Hebu tuone mkono wako. Nadhani nyote mnaninii . . . Yapata—yapata mmoja ama wawili.

121 Sasa, kama Yesu Kristo anabaki yeye yule jana, leo na hata milele . . . Katika Kitabu cha Yohana Mtakatifu, alikutana na mwanamke, Yeye akiwa ni Mwanamume, alikutana na mwanamke, yule mwanamke kisimani niliyehubiri juu yake yapata dakika chache zilizopita, Naye akamwomba maji anywe, Naye akaendeleza mazungumzo naye, baada ya kitambo kidogo, akapata shida yake ilikuwa ni nini. Ni wangapi wanaojua ilikuwa ni nini? Hakika, alikuwa akiishi katika uzinzi. Akasema, "Nenda kamwite mumeo."

Akasema, "Sina yeyote."

Kasema, "Umesema kweli, kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye siye mume wako."

122 Sasa, Mafarisayo walimsikia akifanya hivyo, na kumwona akifanya hivyo, Mwamba uo huo, nao wakasema, "Mtu huyu ni Beelzebuli, ibilisi." Hiyo ni kweli? "Aina fulani ya mpiga ramli wa kisiri, au kitu fulani."

123 Yesu akasema, "Nitawasamehe hilo, lakini siku moja," Maneno kama haya, "wakati Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, ukinena neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe," (Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli?) "ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao."

124 Kwa sababu walimwita Roho wa Mungu Roho mchafu, kama roho wa ibilisi, mpiga ramli. Mtu yeyote anajua kwamba kupiga ramli ni kwa ibilisi. Bila shaka. Hayo yote ni uchawi, na wapiga ramli, na telepathia ya kiakili, na upuuzi wote wa namna hiyo, unatoka kwa ibilisi.

125 Lakini kumbukeni, Yesu alisema katika siku za mwisho wakati tunapokuwa na mawazo haya yote mazuri hapa ya watu mbalimbali, na telepathia ya kiakili, na—na upuuzi huo mwingine waliojaribu kushtaki . . . Ilikuwa ni kitu gani? Utambuzi wa hisia na yote hayo, hayo ni ya ibilisi, nayo Biblia ilisema yangekuwa hapa, "Kama vile Yambre na Yane walivyoshindana na Musa, vivyo hivyo hawa wataipinga ile kweli." Ukweli ni ubatizo wa Roho Mtakatifu na nguvu za Mungu.

126 Yesu alisema, "Watafanana sana, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini." Lakini haiwezekani kuwapoteza walio Wateule, maana walichaguliwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo. "Wale aliotangulia kuwajua, amewaita; wale aliowaita, aliwahesabia haki; wale aliowahesabia haki, tayari amewatukuza." Hiyo ni kweli.

127 Sasa, huyu hapa mwanamke, sijawahi kumwona, kadiri nijuavyo nadhani hatufahamiani. Vema. Huyu hapa mama, sijapata kumwona, labda ni wa rika yangu, labda nimemshinda umri. Lakini hatujawahi kuonana, na hii ndiyo mara yetu ya kwanza kuonana.

128 Sasa, kama Yesu Kristo anabaki yeye yule, naye ameahidi ya kwamba angewaonyesha Mataifa...Nitalisema namna hiyo ili...Mkitaka nilieleze ningeweza, lakini nina hakika mnalielewa. Aliahidi ya kwamba angewaonyesha Mataifa, kama tu vile alivyowaonyesha Wayahudi na Wasamaria, mwishoni mwa wakati wa Mataifa, angewaonyesha Mataifa (Ni wangapi wanaojua jambo hilo?) ishara ile ile, ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi aliyefufuka.

129 Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, wakati Bwana Yesu alipokuwa kule, Mungu aliyedhihirishwa katika mwili alimwambia Ibrahimu mke wake alikuwa ni nani, na jina lake lilikuwa nani. Alikuwa hemani nyuma Yake, Naye akamwambia atapata mtoto kwake, naye akacheka, Yeye akasema, "Kwa nini akacheka?"

130 Sasa, Yesu alisema jambo lilo hilo litatukia kabla tu ya Yeye kuja. Tuko kwenye mwisho wa safari. Sasa, kama Yeye angali ni Masihi yeye yule, Yeye atafanya ishara zile zile za Masihi kujithibitisha Mwenyewe. Mimi si Yeye, mimi ni ndugu yenu tu, mimi ni kama tu ninyi, mtu ambaye amempokea Roho Wake.

131 Sasa, kama huyu mwanamke hakuamini, haidhuru yaliyosemwa, yasingemsaidia kamwe, kwa vyovyote vile. Naye hana budi kuamini kabla jambo lolote halijatukia.

132 Sasa, ninyi huko nje kwenye kusanyiko, amininі tu vivyo hivyo kwa ajili yenu wenyewe, ama kwa ajili ya mtu mwingine, haidhuru ni nini, wewe amini tu kwa ajili yao, uone kama halitukii vivyo hivyo hasa.

133 Sasa, njoo huku kwa dakika moja tu, mama. Sasa, sisi hapa, ninawatakeni tu mpate jambo hili. Hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana maishani, sikujui, bali Mungu anakujua. Ndio kwanza niseme, ya kwamba Mwamba huo ni ule ule jana, leo, na hata milele. Unaamini hilo? Naam. Wewe ni Mkristo, hisia ya roho yako inaniambia wewe ni Mkristo, kama sivyo, ungevuta nyuma.

134 Sasa, sijui uko hapa kwa sababu gani, huenda uko kwa niaba ya mtu mwingine, huenda uko kwa ajili ya fedha, huenda uko kwa sababu ya shida ya kinyumbani, huenda wewe ni mgonjwa, hu—huenda una majonzi fulani, ama kitu fulani, sijui. Lakini umenijia kama mtumishi wa Mungu, kujaribu kuzungumza kupitia kwangu, kama walivyofanya katika Agano la Kale kupitia kwa manabii, kuona ilikuwa ni kitu gani, na kadhalika (Hiyo ni kweli?), kile ambacho kingetukia. Vema basi, kama Yeye angali anabaki vile vile kama alivyokuwa, basi Roho Wake yuko

ndani yetu, na atafanya tu kama Yeye—Yeye alivyofanya wakati huo, hiyo ni kweli?

135 Ni wangapi kwenye kusanyiko wataamini sasa, kwa moyo wenu wote? Vema, jambo pekee ninaloomba, angalieni tu huku, msiwe na shaka.

136 Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Hilo ni zuri. Na kama hatujawahi kukutana, na una shida fulani, ingembidi Mungu kuniambia, au inambidi kuwa na namna fulani ya nguvu ambazo zingeniambia, kwa sababu hakuna njia kwangu kujua. Halafu kupitia hilo, kama ingekwambia, ingekusaidia, sivyo? Ingekusaidia.

137 Vema, uko hapa kwa ajili ya uponyaji, na huo ni tumboni mwako. Una ugonjwa wa tumbo, matatizo, na mambo mengi mabaya kwako. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa, kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

138 Sasa, unaamini? Unaona? Mnaona jinsi Roho Mtakatifu alivyo halisi?

139 Sasa, hiyo ni kweli. Sasa, kama utaninii. . .Ngoja, kuna jambo lingine. Ana jambo lingine akilini mwake, anawazia jambo fulani.

140 Hivi Yesu alitambua nini yao, kitu gani? [Kusanyiko linasema, "Mawazo."—Mh.] Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo nilivyolichukua hilo wakati uo huo, yeye ana jambo lingine akilini mwake. Hiyo ni kweli kabisa.

141 Huyo ni mume wako. Yeye ni mgonjwa, yuko hapa, anahitaji uponyaji pia, sivyo? Wewe hutoki hapa, wewe ni Mkanada. Rudi nyumbani, chukua hiyo leso uliyoimwagia hilo chozi, nyote wawili mtapata afya. Nenda, amini kwa moyo wako wote, katika Jina la Bwana. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

142 Unaamini? Ni rahisi hivyo, yeye anaponywa tu. Sasa kumbukeni, nisingeweza kufanya hivyo, nisingeweza kufanya hivyo bure, ni Mungu. Mnaona? U—unahofu Mungu yuko mbali sana mahali fulani, Mungu yuko papa hapa, Yeye yuko moja kwa moja karibu nawe. Sema tu Naye, Yeye ndiye Mwamba. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

143 Nadhani hatufahamiani.

144 Sasa, kama ukichukua mstari huu namna hiyo, sina budi tu kuharakisha hili kupitia hapa, mwajua. Hiyo ni. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

145 Kuwa tu na imani, usiwe na shaka. Amini kwa moyo wako wote. Sasa, wewe, na—nadhani una umri mkubwa kidogo kuliko wangu. Lakini hatufahamiani, Mungu anatujua sote wawili. Na kama Yeye ataniambia shida yako, ama jambo fulani ulilofanya, ama kitu kama hicho, kama akikwambia yale ambayo yamekuwako, unajua kama hiyo ni kweli ama si kweli, basi ungeweza kujua yatakayokuwako. Hiyo ni kweli?

146 Hiyo ni sawa, kusanyiko? Sasa, hebu tuchukue wawili ama watatu ili. . .Biblia ilisema, "Kwa vinywa vya mashahidi wawili watatu, kila neno na lithibitike." Na ndipo tutaanza tu kuwaombea wagonjwa wanapoendelea mbele. Je, mnaweza kuona Roho Mtakatifu yupo?

147 Sasa, sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu. Lakini Mungu anakujua. Lakini kama Yeye ataniambia shida yako ni nini, utajua kama ni kweli ama si kweli. Unaugua ugonjwa wa figo, hiyo ni kweli, ni mafigo. Hiyo ni kweli. Na jambo lingine, una kivimbe unachoombea. Hiyo ni kweli. Unaamini Mungu anaweza kuniambia hicho kivimbe kiko wapi? Ingekusaidia? Kiko upande wako wa kulia. Hiyo ni kweli, sivyo? Uh-huh.

148 Wewe pia hutoki hapa, unatoka nchi yenye milima, kama vile, Pittsburgh, Pennsylvania. Jina lako ni Bi. Colt. Rudi nyumbani na uwe mzima.

149 Sasa, unapendaje jambo hilo? Je, hiyo ndiyo. . .?. . .Vema, iweni tu na imani. "Kama unaamini!" Amini tu, mwamini Mungu.

150 Vema. Hatufahamiani, nadhani. Sasa, huyu hapa mwanamume. Sasa, hebu tuone. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

151 Aliamini, akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli."

152 Sasa, Mwana yuyo huyo wa Mungu hajafa, Yeye anaishi hapa alasiri ya leo. Sasa, Mungu na atusaidie. Sijui, huenda asimwambie mtu huyo chochote, sijawahi kumwona, sijui ya kwamba atamwambia. Lakini natumaini atafanya hivyo. Nafikiri, hii ni nini, mbili ama tatu? Tatu? Halafu mtu huyu atakuwa ni wa tatu. Vema, wanawake wawili, mwanamume huyu atakuwa wa tatu, thibitisho. Vema.

153 Bwana, Mungu anajua yote kukuhusu, mimi sijui. Lakini kama anaweza kuniambia jambo ambalo unajua silijui, je, ingeisaidia imani yako?

154 Je, ingemsaidia kila mwanamume huko nje kuliamini sasa, kila mmoja wenu ninyi wanaume?

155 Shida yako iko kwenye koo lako, ni umio. Umeenda kwa madaktari, wanataka ufanyiwe upasuaji kwa ajili yake. Jambo ndilo hilo.

156 Hilo ndilo tatizo lake, hilo ndilo lililotukia kabla hajaja kanisani. Unaamini? Naam, bwana.

157 Ilitokea tu niliona jambo lingine nilipokuwa nikihisi roho yako. Hujawahi kuridhika na tukio kama Mkristo bado, kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu. Unamhitaji Yesu kama Mwokozi wako. Hiyo ni kweli. Je, utamkubali sasa hivi kama Mwokozi wako binafsi? Unayatoa maisha yako Kwake?

158 Ninaona huwezi kula, huwezi kumeza vizuri. Hiyo ni kweli. Unafifia tu, unaisha. Hiyo ni kweli. Hilo limekuwa likiendelea kwa muda mrefu sana, linakusumbua kooni mwako. Hutoki hapa, unatoka Cincinnati, Ohio. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Nikikwambia wewe ni nani kwa Roho Mtakatifu, itakusaidia? John Huff, rudi nyumbani ukapone. Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini kwa moyo wako wote?

159 Maskini mtu huyo aliyeketi hapo chini akitaka kuacha kuvuta sigara, unaamini Mungu atakupa shauku yako, bwana? Vema, hutavuta sigara tena, Yesu Kristo anakuponya. Huna kadi ya maombi, sivyo? La, huna kadi ya maombi, huihitaji.

Unamwamini Mungu? Unaamini?

160 Huyo msichana aliyeketi moja kwa moja huko nyuma akimwombea rafiki yake huko Pennsylvania, hiyo ni kweli, huna kadi ya maombi, sivyo? Lakini unamwombea rafiki aliyeko Pennsylvania, nimeona hiyo safu ya milima. Amini kwa moyo wako wote, naye atapona, ni mmoja wa wapendwa wako. Amini kwa moyo wako wote, utapona.

161 Unaamini kwa moyo wako wote? "Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana." Haleluya! Unaamini?

162 Maskini huyo mama aliyeketi huko nyuma akiomba, ana mishipa iliyovimba, jambo la kwanza, naye anamwombea mumewe, yeye huvuta sigara na kunywa pombe pia. Hiyo . . . Huna kadi ya maombi, sivyo, mama? Lakini ulikuwa ukiomba Mungu akusaidie, hiyo ni kweli? Wewe pokea uponyaji wako, mwamini Bwana Yesu Kristo kwa yaliyosalia.

163 Mwamininі Mungu, msiwe na shaka. Ninawapa changamoto kumwamini! Amina.

Nisiposema neno moja, nikuwekee tu mikono, unaamini ungepona?

Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe.

164 Kama nikikwambia shida yako, je, utapona? Ugonjwa wako wa moyo umeponywa, nenda ukapate afya. Amini kwa ninii yako yote . . .

Nisiposema lolote, utaamini kwa moyo wako wote? Njoo hapa.

Katika Jina la Yesu, nenda ukaponywe.

165 Amini. Nyote mnaamini sasa? Je, kila mtu anaomba? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Watu wenye kadi za maombi, watu wasio na kadi za maombi kwenye kusanyiko, popote ulipo, mwamini Mungu, sema na Mwamba.

Katika Jina la Bwana Yesu, ndugu yetu na aponywe. Amina.

Katika Jina la Bwana Yesu, dada yangu na aponywe.

166 Kuna Kitu fulani hapa kinachoniambia mambo haya.

167 Unaamini shida yako ya kike imeondoka? Nenda zako, na useme, “Asante Bwana.” Bwana asifiwe.

168 Unaamini wasiwasi wako ulikuacha? Nenda zako ukaninii . . .Bwana asifiwe.

Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Amini.

Katika Jina la Yesu Kristo, ndugu yetu na aponywe.

Sasa kuwa na imani, amini tu kwa moyo wako wote.

Mungu ambariki huyu mtoto na kumponya, katika Jina la Yesu.

Njoo, mvulana mdogo. Unaamini sasa?

Bwana Yesu akuponye, mwanangu, na akupe afya. Amina.

Njoo dada, mpenzi, njoo moja kwa moja. Unaamini sasa kwa moyo wako wote utapona?

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Njoo ukiamini sasa, usiwe na shaka.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Njoo, ndugu yangu mpendwa.

Katika Jina la Bwana Yesu, ibilisi huyu na akuache, nawe uende ukaponywe.

Mungu ambariki huyu mtoto, pia, katika Jina la Yesu, naomba.

Ni tezi yako, mtu yeyote anaweza kuona hiyo . . .?. . .

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina. Nenda ukiamini, sasa.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Njoo ukiamini.

Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe.

169 Je, kila mtu anaomba? Kila mtu kwenye maeneo ya maombi? Vema.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe. Tujalie, Bwana.

Njoo, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe. Amina.

Katika Jina la Yesu Kristo, mwanamke huyu na aponywe.

Njoni.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Hivyo ndivyo ilivyo, dada, ndivyo ilivyo.

Hiyo hapo aina ya imani inayohitajika kupata baraka.

Katika Jina la Yesu Kristo, naomba uponywe. Amina.

Njoo, dada.

Katika Jina la Yesu Kristo, na uponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, na uponywe.

Njoo, dada. Amini kwa moyo wako wote sasa, nawe utaupata.

170 Katika Jina la Yesu Kristo. . .Usiwe na shaka, kama vile Bartimayo alivyokuwa huko langoni. . .Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

Njoo, dada mpendwa. Usitie shaka sasa, amini ya kwamba itatendeka.

Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aponywe.

Njoo, ndugu.

Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

Katika Jina la Bwana Yesu, uponywe.

Katika Jina la Yesu Kristo, uponywe.

171 Ngoja kidogo tu. (Hilo ni sawa, ni—nilifikiri ilikuwa ni kitu kingine.) Vema, unaamini? Ninyi nyote mnaamini kwa moyo wenu wote? Kila mtu anaamini? Sasa angalieni, mnaona, kama upako upo hapa, watu wakipita, huko ni kuwawekea tu mikono, jinsi hasa ilivyo sikuzote. Roho yeye yule yupo hapa, hivyo tu, si lazima uwaambie watu.

172 Hapa, huyu ni, ninaamini ndiye mtu wa kwanza mweusi ambaye tumekuwa naye jukwaani leo, ninaamini, kadiri nijuavyo mimi. Vema, angalia, siku moja huko Yerusalemu, kulikuwako na msalaba wa kale, unaoparuza, ukikokotwa barabarani, ukikokota nyayo zilizojaa Damu ya huyo Mbebaji. Ndipo Simoni, Mkirene, akamsaidia kuubeba msalaba alipoanguka chini ya mzigo huo, alikuwa Mwethiopia, ambako watu wenu walitoka, Yeye angali anakumbuka hilo.

173 Unaamini Yesu yuyo huyo yu hai leo, Naye angeweza kuniambia shida yako ni nini? Unaamini hilo? Inatokea kwamba huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uliponywa jana usiku. Unataka nikuambie uliokuwa nao? Ulikuwa na ugonjwa wa tumbo na—na kisukari, huo ndio ulioponywa.

174 Jambo lingine, uko hapa kwa ajili ya binti yako. Naye binti yako ana ugonjwa wa tumbo. Jina lako ni Bibi Wells, unaweza kwenda zako nyumbani, na upate afya, katika Jina la Bwana Yesu. Vema.

Njoo ukiamini, usiwe na shaka, kuwa na imani.

Bwana, katika Jina la Yesu, mponye mwanamke huyu na umpe afya.

Vema.

Mungu, katika Jina la Yesu, mponye ndugu yangu na umpe afya.

Sasa, kumbukeni tu, upako wa Roho Mtakatifu ungali hapa.

Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, mponye dada yetu na umpe afya.

Baba uliye Mbinguni, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumpa afya.

175 Njoo, ndugu. Unaamini kwa moyo wako wote? Maskini mgongo huo utakuwa sawa sasa, endelea tu, mwamini Mungu kwa moyo wako wote, na upate afya. Vema.

176 Njoo. Sasa, huonekani kama unayo, bali una yabisi kavu. Lakini unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema, bwana. Unaweza kuupokea, kama ukiamini. Vema, nenda zako, ukishangilia, na useme, "Asante."

177 Mtu huyu ametiwa uvuli wa mauti, kansa. Unaamini Mungu anaweza kuiponya kansa hiyo, bwana?

178 Wote walio huko nje wanaougua kansa, simameni kwa miguu yenu. Kila mtu aliye na kansa jengoni, simama kwa miguu yako.

179 *Usithubutu* kusimama, tayari umeponywa. Amina.

180 Haleluya! Mnampenda?

181 Mama huyu aliyeketi hapa akimwombea mumewe, ana shida ya macho, pia hajaokoka. Unaamini Mungu atamshughulikia, atayaponya macho yake, na kumpa afya? Vema, Mungu akubariki. Jalia Roho Mtakatifu aje juu yake na kumwokoa na maisha ya dhambi.

182 Moja kwa moja nyuma yako hapo, unamwombea rafiki aliye hospitalini, anayekufa, yule msichana. Unaamini kwa moyo wako wote? Vema. Mnaona, ninyi nyote hamna kadi za maombi, hamzihitaji. Kama utaamini, Mungu atauzuia mkono wa mauti.

183 Ninawatakeni tu mjue ya kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa. Amina.

184 Mungu akubariki, ndugu. Mnaona hiyo ni nini? Kama ningeweza kukuponya, ningefanya hivyo. Siwezi kufanya hivyo, bali ninaamini ya kwamba Mungu atayasikia maombi yangu, nawe je? Basi ninamtoa ibilisi huyo mchafu, katika Jina la Yesu Kristo. Nenda, ukaponywe.

185 Hapa, dada, sikujui. Kuna wengi sana wanaovuta huko nje sasa, imenidhoofisha sana hata sijui mahali pa kusimamia. Unaugua ugonjwa wa wanawake, ugonjwa wa kike. Simama papa hapa kwa dakika moja tu.

186 Kila mwanamke huko nje anayeugua ugonjwa huo wa kike, simama kwa miguu yako sasa hivi. Simama kwa ajili ya maombi. Hebu kidogo.

187 Vema, hapa, ulikuwa na jambo lile lile, mama, kwa hiyo wewe simama papa hapa, na uamini kwa moyo wako wote.

188 Vema, angalia hapa, dada, hebu kidogo, una ugonjwa wa tumbo. Simama papa hapa upande huu.

189 Kila mtu aliye na ugonjwa wa tumbo, simama. Amini, usiwe na shaka.

190 Kijana, angalia huku, unaumwa na mgongo. Simama papa hapa.

191 Kila mtu aliye na ugonjwa wa mgongo, simama kwa miguu yako. Mwaminini Mungu. Tumbo lako . . . Sasa, unaweza kusimama upande huu. Mwamini Mungu, amini.

192 Papa hapa pia, wasiwasi.

193 Vema, wote walio na shida ya wasiwasi, simameni kwa miguu yenu. Kila mtu anayesumbuliwa na ugonjwa wa wasiwasi, simama. Vema.

194 Njoo sasa. Hebu tuone ni nani, huyu anayefuata . . . Ugonjwa wa pumu.

195 Wote walio na pumu, simameni kwa miguu yenu, kila mtu simama kwa miguu yako. Mtauona utukufu wa Mungu.

196 Njoni, ugonjwa wa tumbo na wasiwasi simameni upande huu. Vema.

197 Haya basi. Ningewezaje kuwaita hao wote? Lakini Roho Mtakatifu anajua yote kuwahusu. Ni wangapi walio na aina yoyote ya ugonjwa? Simama kwa miguu yako, sijali ni nini, aliye na ugonjwa wa aina yoyote. Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Uko tayari kuunenea Mwamba?

198 Sasa *wewe* nenda ukaamini, *nawe* uende na uamini sasa. Simameni papa hapa kwa dakika moja tu, sasa mwinulieni Mungu mikono yenu, sisi sote.

199 Ninamwamuru ibilisi, katika Jina la Yesu Kristo, Mwamba wetu wa wokovu, aondoke kutoka kwa kila mgonjwa na anayeteseka humu ndani! Ninafanya hivi kwa Damu ya Yesu Kristo, chini ya Upatanisho kwa huduma ya Malaika aliyenituma kufanya ishara hizi na maajabu mbele zenu, kuzungumza juu ya kuja kwa Yesu Kristo.

200 Ee Mungu wa Mbinguni, Muumba wa vitu vyote vyema, tuma baraka Zako juu ya hawa watu huku nikizihukumu hizi nguvu za ibilisi ambazo zimewafunga. Watu hawa jukwaani, wale walio katika kusanyiko, jalia ibilisi awaache, jalia kila kivuli cha kutokuamini kiondoke sasa. Jalia wanene na Mwamba sasa hivi kuhusu ugonjwa wao, na jalia Mwamba umwage nguvu Zake za uponyaji na utukufu miilini na nafsini mwao, na kuwaponya.

Katika Jina la Yesu Kristo, ninawakabidhi kwa Mungu. Amina.

60-0612 Sema Na Mwamba Huu
Miami Valley Chautauqua Campgrounds
Chautauqua, Ohio Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.



Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org